https://dspace.org/

Ni Mvita ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mitaa ya Mambasa, Kenya

Karama, Mohamed

2021
East African Journal of Swahili Studies
https://doi.org/10.37284/2707-3475
Karama, M. (2021). Ni Mvita ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mitaa ya Mambasa, Kenya. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 3(1), 78-90.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

East African Journal of Swahili Studies, Volume 3, Issue 1, 2021
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 3, Issue 1, 2021
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mit^{h}aa ya Mambasa, Kenya

Mohamed Karama

[1] Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030 - 20200, Kericho, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

Tarehe ya Uchapishaji:

27 Juli 2021

Istilahi Muhimu:

Mambasa, Mvita, Toponimi, Isimu, Swahili, Mombasa.

IKISIRI

Miji yoṯ^{h}e ulimwenguni imepawa majina ili kuitambulisha. Majina haya ni hazina ya mapisi na uṯamaḏuni kuwahusu wakaaji wa miji hiyo. Namna inavoitwa, fasiri na fasili za majina hayo husema mengi kuhusu maana na nyusuli zake. Makala haya yamechunguza toponimi ya baadhi ya mit^{h}aa ya mji wa Mambasa, Kenya. Madhumuni yalikuwa ni kuchanganuwa nyusuli za majina kwa kubainisha ṯafauṯi za kimaṯamshi ya majina hayo, kuthibiṯisha kuwa ṯafauṯi hizi zaleta ṯafauṯi ya maana ya majina, na kwamba toponimi za mit^{h}aa hiyo imeelemeya kwelezeya maumbile ya mazingira ya mahali hapo jambo linaloshuhuḏiwa katika jamii nyengine za Kibantu, Kenya. Tulitumiya Ṯaraṯibu za Ulinganisho na Toponimi Kina ili kuchanganuliya data yetu. Data yetu tuliipata kwa kuwauliza wazee wa miyaka 50 na zaidi ambao wana maelezo simulizi kuhusu fasili za majina hayo na data ya upili. Kwa kulinganisha na lugha za jamii zinazokaribiyana za Kimviṯa, Kimijikenra, Kipokomo na lugha za Kibantu kuṯoka bara Kenya tuliweza kung'amuwa kuwa majina haya ya Mambasa yanashabihiyana na yale ya lugha nyengine hivo kutupa ufunuwo mpya kuhusu maana za majina hayo. Tumepata kuwa uṯamkaji wa majina unaleta ṯafauṯi ya maana na hivo usuli wao piya ni ṯafauṯi na ilivozoweleka. Tumepata kuwa majina ya kale yaliitwa kutegemeya maumbile ya mazingira na majina ya mit^{h}aa ya kisasa yameelemeya zaidi vitu au majengo yaliyoko hapo. Kupitiya makala haya tunaamini tumeṯowa fasili mpya kuhusu mit^{h}aa hii na hivo kuwapa fikira nyengine wataalamu wa Chimbo, Uṯalii na Isimu kuhusu majina haya na historiya inayobebwa na majina haya.

APA CITATION

Karama, M. (2021). Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mit^{h}aa ya Mambasa, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *3*(1), 78-90. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368.

CHICAGO CITATION

Karama, Mohamed. 2021. "Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mit^{h}aa ya Mambasa, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 3 (1), 78-90. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

HARVARD CITATION

Karama, M. (2021) “Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mitʰaa ya Mambasa, Kenya”, *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), pp. 78-90. doi: 10.37284/eajss.3.1.368.

IEEE CITATION

M. Karama, “Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mitʰaa ya Mambasa, Kenya”, *EAJSS*, vol 3, no. 1, pp. 78-90, Jul. 2021.

MLA CITATION

Karama, Mohamed. “Ni Mviṯa ni Mvita?: Uchanganuzi wa Usuli wa Toponimi za Mitʰaa ya Mambasa, Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 3, no. 1, Jul. 2021, pp. 78-90, doi:10.37284/eajss.3.1.368.

UTANGULIZI

Ṯangu Shakespeare (ca. K17) mpaka Wamitila (1999), Mazrui (2012), haḏi Owino (2019), na juzi Mutua (2021) wameuliza swali ‘Linani jina?’ na kila mmoja ameeleza fasili yake kuhusu mifumo ya kwita majina ya watʰu, mahali au kʰitu. Tukiinukiya tulisomeshwa skuli na tulisoma magazeṯini majina ya miji na nchi: Peking, Bombay, Ivory Coast na baada ya miyaka michache miji hii sasa yaitwa/yaandikwa: Beijing, Mumbai, na Côte d'Ivoire kimṯawaliya. Huku Uswahilini-Kenya, imepita miyaka miya moja ṯangu wanaṯʰi wa Mambasa, wakinukuliwa katika Stigand (1915: ix), waliposhangazwa na maelezo ya maana ya jina la mji wao ‘Mviṯa’ kwamba ni ‘mji wa vita’ ‘kisiwa kilichojificha’, ‘mji wa ncha’. Tukiyengezeya, nyanjani, kuna wanaosema usuli wa jina ‘Mambasa’ ni ‘min bas’, ‘mambo sasa’, na ‘mwambadze’. Ni dhahiri majina yana umuhimu wa kumtambulisha mtʰu kule aṯokako, lakini piya uṯamkaji, kama tuṯakavothibiṯisha, wa jina hilo una mchango katika utambulisho huwo. Ṯaraṯibu ya kuchanganuwa etimolojiya ya toponimi inafafanuwa kuwa majina ya mahali huṯokana na mazingira au matukiyo muhimu yanayonasibishwa na mahali hapo. Katika makala haya, tuṯatumiya ṯaratibu hii kutatuwa mḏangano na kwangaziya mwelekeyo wa nyusuli za majina ya kale ya mitʰaa ya Mambasa.

Kupitiya maanḏiko tumejuwa Mambasa ilikuwa ikiitwa Kʰongoweya, Mviṯa, Jimbo, Gongwa, Nyali Kʰuu, Nuhasi, Mji wa Kale (Abdulaziz, 1979:146). Naye Muyaka bin Haji katika Abdulaziz ametupa majina ṯafauṯi ṯafauṯi ya mji huu kiushairi bila kugusiya nyusuli za majina hayo. Maelezo ya Abḏilatif Abḏalla (mazungumzo naye kwa WhatsApp, April 25, 2019) yanaeleza baadhi ya nyusuli za majina ya Mambasa na Mviṯa kulingana na maanḏiko yaliyoko, kwa mfano, ‘nabasa’ (kusema hadharani) na ‘Manpasa’ kulingana na James Kirkman, Shihabudin Chiraghdin mṯawaliya. Tunakubaliyana naye kuhusu namna ya kwita majina lakini kuhusu nyusuli maelezo yake hayakubaliyani na uṯaratibu wetu wa uṯafiti kama tuṯakavoonesha. Kazi ya Owino (2019) imeeleza kuhusu athari na ṯahadhari za kisheriya zilizoko katika kwita majina haswa ya watʰu na bidhaa. Mazrui (2012) na Mutua (2021) wameangaziya siyasa iliyomo katika jina la mahali lakini ya Mutua imefanana na yetu kwa kwangaziya maswala ya toponimi ya jina ‘Kenya’ kiuṯamkaji wake; sisi hatuṯomili katika siyasa. Wamitila (1999) ameeleza fasili ya jina ‘mvita’ kwa mnasaba wa kazi za kifasihi na ameṯowa etimolojiya ya jina hili kiuhusika na wala si jina la mahali. Kazi ya Makoti (2007) imeeleza kuhusu anthroponimi kulingana na Wadigo na ikatufunuliya namna etimolojiya ya majina ya watʰu ya Kidigo yalivo na umuhimu katika uṯamaḏuni na mapisi yao. Kazi ya odonimi ya Wanjiru na Matsubara (2017) imetufunuliya kuhusu uhifadhi wa historiya ya nchi na umuhimu wa historiya hiyo katika kujenga uṯaifa kuṯokana na kwita majina ya barabara muhimu katika mji, haswa miji mikuu. Kazi ya Nzasu na Odongo (2014), kiṯabu cha kiyada cha Ḏarasa la 4 katika skuli za msingi, kimegusiya, kwa muhṯasari sana, pengine kwa kiwango cha walengwa, mas’ala ya aina za wakaaji katika mji wa Mambasa, ṯamaḏuni zao, sifa za kijiografiya za maeneo ya mji huu na maenreleo yaliyomo. Kazi hii haikutaja wala kuṯowa historiya angalau fupi ya mji huu mkongwe au toponimi yake. Karama (2021) inayohusu toponimi ya ‘Swahili’ imetupa fikra ya kwangaliya majina haya kwa kurejeleya nadhari ya Kiafrika baḏala ya kuwona kwamba majina haya ameṯokana na kubanrikizwa kuṯoka nje ya uṯamaḏuni wa Waswahili, chembelecho Nurse na Spear (1985). Fasili tulizopata nyanjani zimedhihirisha kuwa mtʰaa au mji Mviṯa huṯamkwa namna mbili: Mviṯa na Mvita. Uchanganuzi wetu umethibiṯisha kuwa pana ṯafauṯi ya uṯamkaji na hivo yanaathiri maelezo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

ya nyusuli za jina hili nriposana twauliza, ‘Kunani na uṯamkaji jina?’

Naṯija ya makala haya miyongoni mwao ni kuṯowa maelezo mengine kuhusu maana ya majina ya mji huu ili kwonrowa mḏangano uliyoko, mfano wa Sacleux (1939: 632), Stigand (khj.) na Kresse (2007: 64). Fauka ya hayo, maṯokeo ya uṯafiṯi wetu yaṯawasaidiya waṯaalamu wa ElimuChimbo kufunukiwa na mapisi ya mahali wanapochimbuwa kama wanavopenḏekeza waṯafiti Nurse na Spear (1985) na Walsh (2003). Mbali ya kujuwa mapisi ya majina haya, jambo lililojiṯokeza katika uṯafiṯi wetu ni kuwa ṯafauṯi za kuṯamka majina haya nrizo zili(na)zosababisha ṯafauṯi za maana ya majina haya. Hivo basi, pana haja ya kuhifadhi maṯamshi ya wasemaji kinḏi kinḏaki wa lugha ya Kiswahili ambayo yaonekana yana mchango katika kuufahamu vizuri mji huu na mengineo kimapisi.

UṮARAṮIBU WA UṮAFIṮI

Ṯaraṯibu za Isimu Mapisi na za Toponimi zilitumiwa kuchanganuliya data yetu ambayo ni baadhi ya majina ya mit^{h}aa ya mji wa Mambasa. Tulitumiya Uṯaraṯibu wa Ulinganisho (Bynon, 1977; Antilla, 1989; Campbell, 1998) wa visawe katika lugha ya Kiswahili na lugha nyengine za Kibantu jirani ya Kiswahili ili ufanano wa visawe hivo uweze kutufunuliya ufanano wa maana ya majina hayo. Visawe hivi vilichanganuliwa katika haṯi finyu kifonetiki za Kiswahili asiliya jambo ambalo Antilla amesema ni gumu. Walakini, kwa faida ya uchanganuzi wetu, sauṯi hizi nrizo zilizotufahamisha uwamilifu wake na hatuwa hii ni jambo wamelikubali Antilla na Campbell.

Timbo muhimu ya kupata asili ya maneno katika Isimu Mapisi huwa ni kwenye nyaraka za zamani ambazo hutwonesha namna lugha ilivokuwa ikitumiwa na wenyeji wakaṯi wa nyuma (Bynon, 1977). Walakini, Kiswahili ni kati ya lugha ambazo hazikuwa na haṯi zake wala uṯamaḏuni wake haukuhifadhiwa kwa uwanḏishi bali mengi ya maswala mbalimbali ya kijamii yalihifadhiwa nyoyoni mwa wasemaji wake na kupokezwa kizazi baaḏa ya kizazi kwa mdomo. Jambo la maanḏishi, kwanza kwa haṯi za Kiyarabu na baaḏaye kwa Kilatini, ni mambo ya hivi karibuni. Kwa sababu hiyo, wakaṯi wa uṯafiṯi wetu, tulikwenra kwa wazee maarufu kwa mapisi ya Waswahili wa miyaka 50 na zaiḏi haswa ambao hawakuathiriwa sana na Kisanifu. Sampuli hii ya wahojiwa ilitufaa sisi kwa sababu ya kupata maṯamshi na fasili ya kisimulizi kuhusu majina haya. Data ya upili piya ilitumika ili kwengezeya lililokosekana kuṯoka kwa wasailiwa na piya kuchuja tulichopawa na wasailiwa. Uchanganuzi wa data ni wa kisinkroniya na uwasilishaji wake ni wa kimaelezo. Tuliyangaliya namna visawe va lugha hizi vinavofanana na kuṯafauṯiyana bila ya kwangaziya mabaḏiliko ya mpito wa wakaṯi mpaka yakafikiya hali yalivo sasa. Mengi ya yanayoelezewa katika makala haya ni ya kidhahanifu lakini nrivo ulivo uchunguzi wa kisinkroniya – hutizama haliya ya lugha inavotumika katika jamii na kwiyelezeya huku ikirejeleya maanḏiko kupunguza udhahanifu huu (Bynon, 1977). Katika makala haya Kiswahili asiliya inawakilisha maṯamshi ya Kiswahili lahaja na Kisanifu kimetumika kuwakilisha Kiswahili Wasṯani. Tunapotaja lugha nyengine za Kibantu tumetumiya jina la jumla bila kuṯafauṯisha lahaja zilizomo nrani yazo.

Uṯaraṯibu wa toponimi uliyofafanuliwa na Tent (2015) unaonesha kuna njiya mbili za kufanya uṯafiṯi wa kitoponimi. Kuna wa kina ambao hushughulikiya majina asili zake kietimolojiya, kwa kufuwata misingi ya kiisimu, kinyaraka, au kifasiri. Njiya ya pili ni kwangaliya kwa ujumla majina yot^{h}e ya mji huwo na kuhiṯimisha kiṯakwimu kuṯokana na mifumo ya kwita majina hayo katika jamii husika. Katika makala haya tulitumiya njiya ya kwanza ambayo hwangaziya usuli kuṯokana na othografiya (namna lilivoanḏikwa [kwa minṯarafu yetu kusemwa]), kimofolojiya, na kisemantiki kama alivofanya Helander (h.t.). Rose-Redwood na wenzake (2010) wameonesha kwamba uṯafiṯi wa toponimi hauna buḏi kuvuka mipaka ya etimolojiya na kwangaziya mas’ala ya siyasa na hisiya kuhusu majina ya mahali. Sisi tulijikita katika etimolojiya ya kimaumbile ya baadhi ya mit^{h}aa ya Mambasa ambayo nriyo yenye kuleta mḏangano wa nyusuli zake. Tumechaguwa baadhi ya mit^{h}aa kwa sababu ya ukale wake na piya uwafiki wa toponimi hizo katika misingi ya uṯafiṯi wetu na kuṯowa fikra ya uṯafiṯi kwa mit^{h}aa iliyosaliya.

Madhumuni yetu yalikuwa ni: mosi, kuthibiṯisha kuwa majina haya ya kale yanaelezeya zaiḏi vitu va kimaumbile. Pili, kuchanganuwa kiisimu-mapisi (mlinganisho wa fonolojiya, mofolojiya, na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

semantiki ya majina hayo) ili kuvumbuwa kuwa majina haya yamechukuliwa kivengine kimaana na yanaregeya kule kule kwenye majina ya kimaumbile. Tatu, na mwisho, ni kubainisha kuwa majina haya yana mshikamano na toponimi za miji mengine iliyopakana na Mambasa hivo kuyakinisha kuwa lugha hizi za Kibantu (Kumbo la Sabaki) katika Mwambao wa Pwani zina ukuruba wa kiṯamaḏuni, kimapisi, na kilugha kama alivosema Nurse na Spear (1985) na Makoti (2007).

MUKṮADHA WA MJI WA MAMBASA

Mambasa, nrivo usṯahikivo kwitwa kama tuṯakavothibiṯisha katika makala haya, ulibuniwa karne nyingi kabla ya kuja wageni wowotʰe. Yaweza kuwa hiyo *Periplus* ilipomaanisha miji ya watʰu weusi Mambasa ilikuwako ṯayari. Haṯa wasafiri wa Kiyarabu, Al Idris (K 12) na Ibn Batuta (K 14), walipoziṯembeleya sehemu hizi wameitaja miji ya Mambasa na mengineo kuwa imesṯawi (Abdulaziz, 1979). Mji wa Mambasa uko katika kisiwa kwenye ufuwo wa pwaa za Afrika ya Mashariki. Kisiwa chotʰe kimezungukwa na bahari na kiko kwa nrani kimezibika na pʰepo kali zinazopiga uso wa upwa huwo. Kaskazini kimepakana na bara la Kisauni, kusini ni bara la Likoni na Mtongwe, na magharibi kimepakana na bara la Changamwe na kwa mbali kidogo Rabai. Hupokeya pʰepo za kusi zinazoleta mvuwa ya masika na pʰepo za kaskazi zinazoleta ukavu na kiangazi kikali chenye joto jingi. Kuna na maleleji wakaṯi kaskazi inapoikaribisha kusi na kipupwe wakaṯi masika yanapoonroka na kukaribisha mchoo.

Neema hizi za kijiografiya nrizo zilizoifanya banḏari ya Mambasa kuwa mahali pazuri pa kwegesha majahazi ya kutuwa kuleta mali kuṯoka nchi za nje na piya mahali pa kupita kwenra mbele ya safari za baharini. Kazi za baharini zilivutiya watʰu wengi wa kuṯoka nrani barani na piya nchi za ng'ambo: India, Indonesia, China, na zaidi bara Arabu. Mṯangamano huu ulileta jumuiya ya watʰu changamano na piya ulisababisha kila mmoja kupiganiya fungu la uṯawala wa mji huu. Wenyeji walijiṯawala kiukoo na wakijitambulisha kwa mahali waṯokako. Wageni Wareno, Waarabu, Majarumani (waliṯawala Ṯanganyika), Maingereza walikuja na walijitwaliya uṯawala kwa nguvu. Kubakurana huku kuutwaa utawala wa mji huu kulileta vita vikubwa baina ya Waarabu na Wareno, Waarabu na wenyeji, Maingereza na wenyeji.

Ṯangu zamani Mambasa kulikuwako na ukulima mambo ambayo Ibn Batuta hakuwacha kuyataja. Piya waliṯegemeya kuletewa chakula chao kuṯoka miji ya Pʰemba na Nyika (sehemu ya ardhi nrani kidogo ya Mambasa). Nikikuliya mimi kulikuwa na viṯaru Bonreni (ilipo New Peoples Hotel), Kikowani na Allidina vikipanrwa maboga kwa ajili ya kula na kuuza sokoni. Mashamba makubwa yalikuwako kuvuka kisiwa magharibi, kusini na kaskazini mwake hata sehemu hizo zikiitwa 'shamba'.

Leo Mambasa ni mji mkubwa ulopanra cheo na kuwa Mji Mkuu wa Pili nchini Kenya. Ṯena, una banḏari kubwa ya Kilinrini na uwanja wa nrege wa kimaṯaifa. Mashamba mengi yashafekwa na majumba makubwa kuchukuwa mahala pake na mji kupangika kisasa haṯa kukawa na mitʰaa yaitwa Majengo Mapya, Magorofani huko huko kulikokuwa kukiitwa 'shamba'.

MAJINA YA MITʰAA YA MAMBASA

Sacleux (1939:604-5) ameorodhesha mitʰaa ya Mambasa na ameigawa kulingana na ukuruba na ngome ya Fort Jesus, ukale, usasa, na umbali wake na mtʰaa wa zamani wa Mambasa yaani Mji wa Kale. Ametaja Ngomeni Fort Jesus (Kavani); mitʰaa ya Mji wa Kale: Mkunguni, Msalani, Kilifi, Bondeni, Kikoani, Karoleni (Kaloleni); mitʰaa ya hivi karibuni: Makadara (Mtʰaa wa waBulushi), Shehejundani; na mitʰaa ya kanro: Kilindini, Makupa, Mshimanzi, Baraki, Pwani wa Kisauni, Kizingo.

Orodha hii twaiyengeza, kwa faida ya data ya makala yetu, Baghani, Ingilani, Ganjoni, Liwatʰoni, Ziwani, Kiziwi yotʰe ya kisiwani. Halafu kuna Nyali, Kʰongoweya, Mishomoroni, Miyuchi, Bombolulu, Bumburi (siku hizi Bamburi), Uṯange, Maunguja. Upanre wa magharibi kuna Changamwe, Bomu, Mikinrani, Mik(g)adini, Jomvu Kʰuu, Jitʰoni. Kusini kuna Likoni, Mtʰongwe. Mwisho kabisa ni mitʰaa ya hivi karibuni Kerekeṯa, Peleleza, Guraya, na Majengo (King'orani, Mferejini, Chura, Ropa, Sidiriya, Kipera (Floringi)). Tumeengeza mitʰaa hii kimakusudi ili wakaṯi tunapochanganuwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

aina za toponimi tuweze kufahamu kivipi mitʰaa ya kizamani na ya kisasa iliitwa hivo.

Aina za toponimi ya Mitʰaa ya Mambasa

Kulingana na Tent na Slatyer (2009) akinukuliwa na Tent (2015:73) anasema toponimi ni kumbukumbu za kutweleza sisi ni kina nani, lini tulikuja, na ni hazina kʰuu ya habari za historiya ya mahali pale. Katika ṯaraṯibu hii ya uṯafiṯi wa toponimi, Tent amebayanisha aina kadhaa za toponimi na nriyo tuliyotumiya kwelezeya toponimi ya mitʰaa ya Mambasa.

1 Toponimi ya Mnasaba: ni ile inayoashiriya mnasaba wa mahali hapo na mukṯadha wake au kʰitu kilichopo hapo. Kwa mfano, twaweza kusema Lango la Papa, Madhubaha, Lighthouse (Mama Ngina) inanasibishwa na muktadha wa mahali hapo. Kwa mfano, Madhubaha, neno la Kiyarabu kwa maana ya ‘kichinjiyo’, karibu na Allidina School, kaskazini mwa kisiwa huwa pana sherehe ya kuchinja hapo kila mwaka wakaṯi wa Mwaka Mpya wa Waswahili.

2 Toponimi ya Matukiyo: ni inayohifadhi tukiyo, tenro, sherehe fulani, au ṯarehe ya jambo lililoṯokeya hapo. Kwa mfano, Baghani uko karibu na Ngome ya Fort Jesus na jina lenyewe asili yake ni la kiyarabu lenye maana ya ‘vita au mapambano ya kivita’, ‘ujambazi’ au ‘uwasheraṯi’ (Al Mawrid, 1995). Katika sarufi ya Kiswahili tunajuwa kuwa kiyambishi /-ni/ ni mofimu ya kuonesha mahali. Tuṯaona kwamba fafanuzi mbili za mwanzo zaafiki toponimi ya mahali hapo kwa sababu ya ukuruba wake na Ngome, nripo palipopiganwa vita baina ya wananchi wakisaidiwa na Waarabu kumwonrowa Mreno. Baghaa, kwa maana ya uwasheraṯi, maelezo haya hayakubaliyani na wazo letu kwa sababu nrani ya Mambasa kulikuwa na sehemu ikijulikana kwa uwasheraṯi ikiitwa Msufi Mkavu karibu na Mwembe Tayari, lakini, mahali penyewe hapakuitwa kwa kazi ifanywayo hapo bali palipawa jina la kʰitu maarufu kilichokuwako nrani ya mtʰaa huwo, mti wa msufi, vilevile Baghani haiwezi kuchukuwa maana hiyo.

3 Toponimi ya Hisiya: ni ile inayoṯokana na uṯathmini wa hisiya ya mpaji jina mahali hapo au kuna sababu ya mlemeo mkubwa wa sifa ya hapo mahali. Mfano wa toponimi hii ni mitʰaa inayoitwa Kerekeṯa (karibu na Hospitali Kʰuu ya Mkowa, Mambasa) na Peleleza uliyoko Likoni. Kulingana na Kindy (1972) majina ya mitʰaa hii iliṯokana na maṯajiri wawili, Sir Ali bin Salim aliyeliita shamba lake Peleleza (kuchunguza watʰu) na Sheikh Rashid bin Soud Shikely akaliita shamba lake Kerekeṯa (kukereka) kumjibu ṯajiri mwenziye Sir Ali kuṯokana na siyasa iliyokuwa ikienreleya wakaṯi huwo kabla ya uhuru wa Kenya 1963.

4 Toponimi ya Mguro: ni ile inayoelezeya namna mahali panapopata jina lake kuṯokana na mahali kwengine au kʰitu maarufu hapo. Mfano mzuri wa aina hii ni jina Majengo au Mkunguni. Tuṯaona kuwa katika Mambasa kisiwani kuna Majengo aina nyingi ya Ropa (kuṯokana na ngoma ya Simba Ropa nriko iṯokako), Mferejini (palikuwa na mfereji wa kuuza maji hapo), King’orani kwenye king’ora cha kuita watʰu kazini. Ukivuka Daraja la Nyali ukifika Kisauni uṯakuta Majengo Mapya karibu na Msikiti Mkubwa hapo na ukienra haṯa Mṯwapa, Kanamai kuna Majengo. Haṯa nrani ya Nairobi na Kisumu kuna Majengo inayokaliwa zaidi na Waswahili. Hali kadhalika kuna Mkunguni (aina ya mti) Lamu, Mambasa, na Zanzibar. Vilevile, kuṯokana na mti, Matonroni (Lamu) na Mtonrooni Mambasa (karibu na Kibokoni).

5 Toponimi ya Kiasili: ni ile inayoelezeya uwasili wa mahali hapo au neno lenyewe ni la kiasili. Mtʰaa wa Ganjoni uliyoko upanre wa Bandari ya Kilinrini nriyo sehemu asiliya ya Waṯangana na Wakilinrini. Kulingana na mahojiyano yangu na mwanafunzi mmoja wa Uzamifu nilipomuuliza kuhusu Kiganjo, mji uliyoko Nyeri, alinambiya Kikikuyu ‘iganjo’ ni ‘ardhi ya wahenga’ ya jamii yao. Sembuse katika Kiswahili jina hili kuwafikiyana na Waṯangana na Wakilinrini ambao simulizi zao zajinasibisha na huko na makaburi yao yako huko na huzikwa huko wanapofariki duniya.

6 Toponimi ya Maadhimisho: ni inayoelezeya mahali kwitwa kwa kwadhimisha au kumuenzi mtʰu. Katika sehemu iliyoko karibu na Posta Kʰuu ya Mambasa pana mtʰaa hapo waitwa Sheikh Jundani. Pameitwa hivo kwa sababu shekhe huyu aliujenga msikiti maarufu hapo na yeye mwenyewe akazikwa hapo. Ni mahala maarufu Mambasa kwa kuzuriwa makumbusho ya shekhe huyo na watʰu kuomba baraka zake.

7 Toponimi ya maelezo: nriyo maarufu zaiḏi ya zote tulizozungumziya awali. Toponimi hii

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

huelezeya sifa zilizoshikamana na k^{h}itu kilichopo katika mahali hapo. Sanasana huwa k^{h}itu cha kimaumbile ambacho huipa sura sehemu hiyo kuṯokana nacho. Kwa mfano: mto, msitu, mlima, ardhi k^{h}avu, ardhi ṯambarare, bonre, shimo, ziwa au kidimbwi. Katika sehemu hii tuṯachanganuwa toponimi za mit^{h}aa ambayo baadhi ya fafanuzi tulizozipata nyanjani hazikubaliyani na uṯaraṯibu wa kuṯafiti toponimi kwa kuwa zimekengeuka na kawaida inayoonekana – toponimi za eneo lote zina sifa iliyokaribiyana ya kwita majina kuṯokana na maumbile. Twaeleza ifuwatavo:

i) Kavani na Kibokoni

Ni majina ya mit^{h}aa ambayo yapatikana katika miji mingine Kavani, Mayotte, Comoros na Kibokoni, Zanzibar. Kresse (2007) na Abdulaziz (1979) wamesema Kavani, mahali palipo na afisi au makazi ya mkuu wa serikali ya wakati wa ukoloni Wareno, uko katika mt^{h}aa mkubwa wa Kibokoni. Tuliyelezwa piya Kibokoni ni mahali palipoonekana/kuwako viboko (wanyama). Kresse akimnukuu Maitland-Jones amesema ni mahali palipokuwa pakichapwa wat^{h}u na mijeledi ya ngozi ya kiboko.

Fasiri yetu ya Kavani ni kuwa katika Kimviṯa /w/ inaweza kuwa /v/ kwa mfano, neno /wewe/ huṯamkwa /veve/ 'you'. Kwa mfanano huu basi twaweza kusema 'kavani' ni 'kawani' ambayo tukionrowa /-ni/ ya mahali iṯakuwa 'kawa' yenye kumaanisha chombo cha miyaa cha kufinikiya chakula; umbo lake ni kama mnara 'cone'. Kulingana na Sacleux 'viboko' ni aina ya mshono wa kanzu kama minara au mrera (mafundi wa kushona nguwo za kike walitwambiya 'mrela' au 'flare'). Kwa hivo, katika mukṯadha huu, kiboko si mnyama, si mjeledi ni mnara na ushahidi ni Kibokoni nriko kwenye misikiti ya minara ya kizamani, Mandhiri (piya wajulikana Msikiti Mnara) na Basheikh, na Fort Jesus yenyewe pambizo zake.

Maelezo ya pili ya Kavani inatokana na 'uvaa' kwa Kit^{h}ikuu, kiwaa kwa Kimviṯa yenye maana ya uwanja mtupu katika eneo lenye miti mingi kama msitu wa 'savannah' (Sacleux, 1939). /ka/ katika Kavani ina maana ya udogo (Ngeli 12) na /ni/ ni ya mahali. Kwa hivo /va/ ni uwanja mtupu katika miti mingi. Nyanjani tuliyelezwa kuwa katika enzi za Wareno kulikuwa na uwanja mkubwa uliyozungushiwa ukuta katika sehemu hiyo ili kujilinra na uvamizi wa wananchi wa Mambasa ambao walikuwa wakiupinga uṯawala wao. Kwa hivo, Kavani ni uwanjani palipokuwa na miti mingi na majumba yaliyojengwa yalizungushiwa uwa wa mawe. Kuṯokana na tafsili hii twaweza kusema piya 'kavani' ni neno lengine linalomaanisha 'uwa', 'ngome', yaani hiyo Fort Jesus au ni huwo mt^{h}aa wa Wareno wenye uwa.

ii) K^{h}ongoweya

Muyaka bin Haji na Ustadh Ahmad Nassir, washairi watajika, woṯ^{h}e wameuwita mji wa Mambasa, K^{h}ongoweya. Ahmad amesema nrilo lililokuwa jina la zamani kabla ya Mambasa. Katika kuuliziya kwetu wasailiwa wamesema vivo hivo na sisi piya twasema toponimi hii ni jina la kale la Mambasa. Ṯafauṯi inakuja tulipowauliza maana ya jina hili. Woṯ^{h}e walisema ni 'kumkaribisha mt^{h}u' katika msemo 'mgeni kongo' yaani 'karibu mgeni'. 'K^{h}ongoweya' kwa maana ya kumkaribisha mt^{h}u kama ilivo haikubaliyani na uṯaraṯibu wetu wa uṯafiṯi.

Tukifuwatiliya makamusi tuṯapata kuwa 'k^{h}ongo' kulingana na Krapf (1882) ina maana ya 'mnazi ulozeeka', 'msitu ulozeeka' na Sacleux amesema ni 'tobwe', 'shimo'. Jina hili K^{h}ongoweya twaweza kuligawanya kimofolojiya /k^{h}ongo- + -e- + -a/. /k^{h}ongo-/ nriyo mzizi wa kitenzi, /-e-/ ni mofu ya kauli ya kutenreya na /-a/ ni kiishiyo. Mohamed (2001) akiyelezeya kuhusu vitenzi va kauli ya kutenreya alisema kuwa mofimu za kauli hii huweza kwelezeya hali ya kuwa – kile kitenro kiko katika kufanyika. Mohamed S. (2001: 80) ametumiya neno 'kudogoweka' kwonesha hali imo katika kufanyika kwa kauli ya kutenreya. Kwa mnasaba huu twaweza kusema kuwa K^{h}ongoweya ni msitu mzee, wenra ukiwa mzee au ulikuwa mbichi sasa wenra ukizeekeya. /w/ na /y/ zilizomo katika maandiko ya jina hilo ni kwa sababu ya kukutana irabu t^{h}atu kwa pamoja ikabiḏi kwengezwe viyayusho hivo katikati yao. Kwengezeya, K^{h}ongoweya kwa maana ya 'tobwe' 'depression' yawezekana kwa sababu ipo sehemu katika eneo hili yaitwa Ziwa la Ng'ombe, panapokusanyika maji makuu wakaṯi wa masika.

Ṯafauṯi nyengine inayojiṯokeza kuhusu jina hili ni kwamba linapoṯamkwa huwa kuna mpumuwo /k^{h}ongoweya/ jambo aliloonesha Abdulaziz (1979)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

wakaṯi alipokuwa akiyaanḏika mashairi ya Muyaka. Huu mpumuwo katika Kimviṯa una uwamilifu wa kuṯafauṯisha maana. Kwa mfano, tukisema /paka/ ni ‘to colour’ lakini tukisema /p^{h}aka/ ni ‘cat’. Wakaṯi tunapoṯamka ‘kongoweya’ kwa maana ya kukaribisha hakuna mpumuwo katika /k/, hivo basi, ni maneno mawili ṯafauṯi hayo; /k^{h}ongoweya/ ni msitu na /kongoweya/ ni kukaribisha mtu.

iii) Nyali

Wakaṯi wa utafiti huu nililibwaga swali la nyusuli za majina ya mji wa Mambasa kwa wanafunzi wangu na wakasema usuli wa jina hili nyali ni ‘miyale(i) mikubwa iliyoṯokana na vita vikubwa vilivopiganwa baina ya Wareno na Waarabu’. Historiya inatwambiya vita viliyenreleya mara kwa mara mpaka 1728.

Kimofolojiya /nyali/ ni wingi wa /mwali/ ambapo Kisanifu ni /miyale(i)/ lakini kilahaja husemwa /nyali/. /mwali/ inafanana na jina la Nchi iliyoko katika Jumuiya ya Comoros inayoitwa Mohéli/Mwali [mɔ.e.li] piya huṯamkika Moëli (Sacleux, 1939:580). Mwali piya huṯamkwa ‘mwalio’ katika lahaja za Kusini (za Tanzania) na ina maana ya kupanga vijiti chini katika mtungi, au kuzipanga nrizi kwenye vijiti hivo (Sacleux, 1939:1014) kama wafanyavo mama zetu wanapozipika. Huku kupanga vijiti piya huitwa ‘uziyo’ kama wafanyavo wavuvi baharini kuwa ni mtego wa samaki. Huu ‘uziyo’ una mnyumbuliko wake kwa maana ya ‘kiziwi’ (na kuna mt^{h}aa Mambasa kwa jina hili) lenye maana hiyohiyo ya ‘uziyo’. Wasailiwa wangu walinikumbusha kuwa pale forodhani mpaka Jiwe la Mbu palikuwako na nyuziyo hizi za kushika samaki. Kuṯokana na fafanuzi hizi yaweza kuwa Nyali K^{h}uu humaanisha nyuziyo k^{h}uu au miti mikuu na yaweza kuwa kwa kwitwa piya K^{h}ongoweya basi palikuwa na msitu mkubwa.

Fasili nyengine tukitumiya jina la Kimijikenra ‘nyari/nyali’ ina maana ya ufunuwo ‘cleft’ (Mgombato, 2004). Kuṯokana na jiografiya ya ulipo mt^{h}aa wa Nyali leo, twaweza kusema ni ile ardhi inayokinga kisiwa cha Mambasa na miji ya nrani katika upulu huwo mpaka kufikiya ufuwo wa Rabai. Kwa minṯarafu hiyo, twaweza kusema nrilo lango k^{h}uu la bahari ya kwingiliya nrani ufikiye mit^{h}aa ya Tudor, Mikinrani mpaka Rabai kwa bahari. Hoja yetu inashikiliya kuwa ni ile ardhi inayokinga miji ya nrani kwa sababu ya umbile la lango na jina tulilopata nyanjani kutoka Mindat (2021) ni Ras Iwetini (Nyali Point) na mkabala wake ni Ras Ṯaka, Maḏobini (Abdulaziz, 1979: 288).

iv) Kaloleni

Hili nrilo jina lililoleta maelezo tata kati ya majina yoṯ^{h}e ya Mambasa. Wasailiwa woṯ^{h}e kutoka wa Kiswahili mpaka wa Kimijikenra na baadhi ya wa Kipokomo walinieleza kuwa maana yake ‘kaangaliyeni’. Na haswa wa Kimijikenra walinipa na historiya-simulizi ya namna mji wa Kaloleni uliyoko Wilaya ya Kilifi ulivokuja kwitwa kwa maana hii. Twaelewa kuwako na maelezo ya aina hii kwa sababu neno ‘kaloleni’ laṯokana na neno ‘lola’ kwa maana ya ‘kuona, kwangaliya’ na wingi wake ni ‘kaangaliyeni’ lakini uṯafiṯi wetu haukukubali fasili hii.

Nadhari yetu ilivutwa na mji katika Wilaya ya Tana River unaoitwa Galole. Mshawasha wetu ni /k/ katika Kiswahili huweza kugeuka na kuwa /g/ kwa mfano katika maneno /kiza/, /keṯe/ huṯamkwa piya /giza/ na /geṯe/ kimṯawaliya. Nilipowauliza wasailiwa wangu wa Kipokomo kuhusu maana ya ‘galole’, neno siyo usuli wa mji, walinijibu kuwa kwa Kiborana na Kipokomo humaanisha ‘mkono wa mt^{h}o’. Na nilipowauliza kuhusu wanauwitaje ‘mt^{h}o’ wakanijibu kuwa huitwa ‘chana’, ‘galana’ ‘tsana’, na mchirizi ‘stream’ unaoingiya mt^{h}o mkubwa huitwa ‘lalo’ ambapo kwa Kimijikenra ‘lalo’ lamaanisha ‘kijiji’ (Mgombato, 2004). Katika fonolojiya hili laelezwa kuwa mfanyiko wa ‘metathesis’ (Campbell, 1998) yaani kuhamishwa sauti wakaṯi wa kuṯamkwa kwake, ya mbele ikaja nyuma na nyuma ikaja mbele. Kwa mfano, katika maneno ‘kibiriṯi/kiribiṯi’, ‘huruma/ruhuma’. Na tukilichukuwa kuwa laṯokana na ‘lola’ basi lawafiki na maana ya Kiswahili kumaanisha ‘kuoga’ ambapo twaikuta dhana ya ‘maji’ ipo hapo. Kwa kushikanisha maelezo ya Kipokomo na Kiswahili kuhusu toponimi ‘Kaloleni’ tuṯaona inahusu mchirizi wa maji (kijit^{h}o). Kuṯokana na maelezo hayo twaweza kukatikiwa kuwa ‘kaloleni’ ina maana ya ‘mahali kwenye mt^{h}o mdogo’ hivo kukubaliyana na ṯasnifu ya kimaumbile.

Mt^{h}aa ambao suala la mt^{h}o lapatikana katika Mambasa ni ule unaoitwa Miyuchi uliyoko katika maeneo ya Mishomoroni. Katika lugha nyengine za Kibantu ‘mt^{h}o’ huitwa ‘oroche’ (Kikisii), ‘usi’

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

(Kikamba), na ‘oluchi’ (Kiluhya). Tuṯaona kuwa majina yoṯʰe matatu yanafanana na jina la mtʰaa huwo wa Mambasa, Miyuchi. Pengine siku za nyuma, au mpaka leo, kuna mtʰo wa msimu wa mvuwa uliyokuwa ukielekeya baharini kwa upanre huwo. Katika sehemu ya Mikinrani magharibi ya Mambasa piya pana mahali paitwa Jitʰoni. Niliarifiwa ni mahali padogo ambapo maji hayakupwi na ni karibu sana na Rabai; watʰu huvuka kila siku kuja kufanya kazi sehemu za Changamwe na kurudi makwao jiyoni. Neno hili ‘tʰoni’ twalipata ṯena katika mtʰaa unaoitwa Liwatʰoni. Kulingana na Sacleux ukurasa wa 435 ‘liwa’ katika Kimviṯa na Kiyamu ni ‘mashamba’ yanayolimwa nafaka na maboga. Kuṯokana na maelezo haya Liwatʰoni /liwa + tʰoni/ ni mashamba ya mtʰoni (pahali pasipokosekana maji katika bahari). Na Mtʰongwe nayo ni majina mawili kushikanishwa /mtʰo + ngwe/. Kulingana na wa Mutiso (2005: 179) wakaṯi alipokuwa akiyelezeya ‘ngwe’ katika *Utendi wa Hamziya* alisema ni ‘kina kirefu’ hivo tuṯaona kwamba mahali ulipo mtʰaa huu ni karibu na bahari ya Bandari ya Kilinrini ambayo humaanisha ‘mtʰo wenye kina kirefu’.

v) Ingilani

Wakaṯi wa kuuliza kwetu kuhusu maana ya jina hili au usuli wake baadhi ya wasailiwa walitwambiya yaṯokana na jina ‘England’ (Wingereza) au ‘ingiyeni’. Shauku yetu ikapatwa na neno la Kibaluhya ‘ing’ani/eng’ani’ lenye maana ya ‘shimo’ na kuna wengine walitwambiya ni ‘kaburi’. Waliweza kuṯafautisha ‘ing’ani’ ambalo ni shimo niya haswa ni kufukiwa maiṯi na ‘eshirindwa’ ni shimo ambalo ṯayari ashafukiwa maiṯi. Lakini katika Kiswahili yaweza kuwa ni shimo ‘depression’ kama tulivosema katika Kʰongoweya. Ing’ani na Ingilani yaweza kuwa ni neno moja kwa sababu /l/ imepachikwa na hili lapatikana katika Kiswahili ‘kulota’ na ‘kuota’ zoṯʰe ni ‘to dream’. Na ithibaṯi ni kwamba mandhari ya ardhi ya mtʰaa huu yaṯakwambiya kuwa ni shimo kwa sababu ukiṯoka Majestic Cinema kwenra Jamaṯini washuka kilima na ukiṯoka Barka Restaurant kuja Island Dishes piya washuka kilima na Ingilani iko chini shimoni.

vi) Mviṯa, Mvita, Mambasa, na Kisauni

Tumekusanya majina haya matatu pamoja kwa sababu yoṯʰe yana maelezo mamoja kuhusu nyusuli zake. Kisauni ni mtʰaa mkubwa uliyoko kaskazini ukishavuka Ḏaraja la Nyali. Nawo Mviṯa/Mvita ni mtʰaa uliyoko magharibi ya kisiwa cha Mambasa na ni jina la Eneobunge. Mambasa ni jina la kisiwa chenyewe mbali ya kuwa ni jina la Wilaya. Muyaka na wasailiwa nyanjani wametaja kuwa Mviṯa ni kati ya majina ya kale ya Mambasa. Picha tulizoziyona katika Makumbusho ya Fort Jesus zinazo jina hili Mambasa japo limeandikwa Mombas(z)a.

Usuli tuliyoupata nyanjani umetweleza kuwa Mambasa ni ‘mambo sasa’, ‘min bas’ (kutoka kwenye shida), ‘manbas’. Mviṯa nayo wengine wametweleza kuwa ‘mji wa vita’ ‘mji wa ntʰa’ (mji wa ncha), ‘mshale na ntʰa’ (mshale na ncha kuṯokana na Kikale ‘mvi’ ni ‘mshale’). Sacleux ametaja piya ‘uvi’ ni mvi nyele nyeupe, mdudu nyigu, na mlango. Kisauni nayo tuliyambiwa ni ‘kilifi/kisasi kisahauni’, ‘kisa cha wahuni’. Fasili zoṯʰe hizi hazikubaliyani na ṯaraṯibu za uṯafiṯi wetu kama tunavoeleza hapa chini.

vi).1 Mviṯa au Mvita? Wamitila (1999) akiyangaziya mas’ala ya kifasihi anaeleza kuwa neno hili ‘mvita’ laweza kuwa na maana ya ‘mapambano’, na, akimrejeleya Sharifa Zawawi, anasema ‘vita’ inaweza kumaanisha ‘maisha’ kwa kuchukuwa maana ya Kilatini. Wazee tuliyowaomba kutweleza maana ya jina ‘mvita’ walilitamka /mviṯa/ na maelezo yao yakawa ni ‘mji wa vita’. Uchanganuzi wetu kuhusu jina hili /mviṯa/ kuṯamkika vengine (ili kusikiya namna inavotamkwa angaliya video ya Hiistoriya) na kwelezwa vengine sisi tuliliyona lina mushkili.

a) Mviṯa ni /mvi + ṯa/: Katika mofolojiya iko mbinu ya kushikanisha nomino mbili kutengeza nomino moja kama ilivodhihiri kwa wasailiwa wetu. Kwa mfano, /msumeno/ inaṯokana na /msu/ ni upanga kikale na /meno/ ‘teeth’, hivo ni ‘upanga wenye meno’. Hivo basi, mviṯa ni mshikamano wa majina mawili /mvi + ṯa/.

b) /mvi/ ni /mu + vi/: Katika Kiswahili, ngeli ya binadamu, mti, na baadhi ya vitu inawakilishwa na mofimu /mu-/ au /m-/. Tunaweza kusema /mu-tu, m-tu/, /mu-ti, m-ti/, /mu-kono, m-kono/, kwa hivo, /mvi/ tunaweza kusema ni /mu-vi/. Tukichukuwa /mu-vi/ na kufuwatiliya usawe tuloeleza katika Kavani tutaona /v/ inageuka na kuwa /w/, hivo tunapata /muwi/, ambalo ni sawa na /mji/ katika Kisanifu. Kwa minṯarafu hii, tuṯakubali maneno aloyasikiya Sacleux kwamba mviṯa ni ‘muwi wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

vita' kwa maana ya 'mji wa vita' japokuwa mwenyewe alikataa fasili hii (Sacleux, 1939:632) nasi ni hali kadhalika. Katika Kimvit̪a /mu-vi/ imedonroshwa /-u-/ na kuwa /mvi/ kama tulivoeleza awali kuhusu kiyambishi cha ngeli hii.

c) Vita ni /viha/: Katika Fonolojiya saut̪i yenye kuleta t̪afaut̪i ya maana katika maneno huwa na umuhimu wa kifonimu. Kwa mfano, tukit̪amka /kaa/ twamaanisha 'kuketi chini' na tukiit̪amka na mpumuwo /kʰaa/ ina maana ya 'mnyama wa baharini'. Vilevile, tukisema /tʰaa/ twamaanisha 'mkoba wa kutiliya vifaa va uvuvi' na tukisema /t̪aa/ twamaanisha 'bulb' ya kuangaziya chumba. Kwa hivo saut̪i /t/ ya ufizini inaleta maana nyengine na saut̪i /t̪/ ya nyuma ya meno ya juu na kwa sababu hiyo /k/, /kʰ/, /t/, /tʰ/, na /t̪/ ni fonimu. Hivo basi majina haya mawili 'Mvit̪a' na 'Mvita' kwa t̪afaut̪i ya kut̪amkwa kwake it̪aleta t̪afaut̪i ya maana ya majina hayo na nyusuli zao.

Kwamba t̪afaut̪i ya kut̪amka husababisha t̪afaut̪i ya maana sasa tweleza maana za saut̪i /t/ na /t̪/ katika majina hayo mawili. Tukiyanza na /t/ tut̪aona kuwa inaafikiyana na maelezo kuwa 'mvita' ni 'mji wa vita'. Kusema hivo ni kwamba /vita/ ile /t/ ni ya ufizini na saut̪i hii hii twaipata kuwa ni /h/ katika Kimijikenra. Kwa mfano:

Kimijikenra	Kimvit̪a	NKisanifu	
/viha/,	/vita/	/vita/	'war/battle'
/muho/,	/mtʰo/	/mto/	'river'
/muhi/,	/mti/	/mti/	'tree'
/muhu/,	/mtʰu/,	/mtu/	'person'
/muhupu/	/mtupu/	/mtupu/	'empty'

Katika mifano hiyo tut̪aona kwamba /t/ ya Kisanifu na Kimvit̪a inat̪amkwa /h/ katika maneno ya Kimijikenra. Kwa mfano /mti/ 'tree' kwa Kimvit̪a na Kisanifu yat̪amkwa 'muhi' kwa Kimijikenra.

d) /ts/ ni /t̪/ na /s/: Tunapokuja katika /t̪/ ya nyuma ya meno ya juu katika Kimvit̪a kisawe chake kinat̪amkwa katika maneno yaliyo na /ts/ katika Kimijikenra. Kwa mfano:

Kimijikenra	Kimvit̪a	Kisanifu	
/mtsanga/	/mt̪anga/	/mchanga/	'soil/sand'
/tsana/	/t̪ana/	/chana/	'to comb'
/tsaha/	/t̪ʰawa/	/chhawa/	'louse'
/mutsi/	/mut̪i/	/mchi/	'pistle'
/mutsi/	/mt̪i/	/mchana/	'day'
/tsalafu/	/siyafu/	/siyafu/	'black ant'
/tsahu/	/satu/	/chatu/	'big snake'

Katika mifano hiyo tut̪aona kuwa /ts/ ya Kimijikenra huwa /t̪/, /s/ katika Kimvit̪a. Katika Kisanifu hugeuka na kuwa /ch/ na mara nyengine hugeuka /s/ mfano, /tsana/ husemwa /t̪ana/ Kimvit̪a na /chana/ 'to comb' Kisanifu. Saut̪i hii /ts/ ya Kimijikenra ni /t̪/ katika Kimvit̪a yamesemwa piya na William Taylor (1891). Ni kweli kuwa /tsa/ katika Kimijikenra piya ina maana ya /ntʰa/ Kimvit̪a na /ncha/ Kisanifu kwa maana ya 'sharp point'. Lakini wasailiwa wetu jina Mvit̪a walikuwa wakit̪amka /mvit̪a/ na wala *si* /mvitʰa/ yenye mpumuwo ambayo ingeleta maana ya 'mji wenye ncha'.

e) /tsaka/, /t̪aka/ ni msitu: Tukishaona kwamba t̪afaut̪i za kut̪amka zinaonekana wazi sasa tuje kwenye ut̪afaut̪ishaji maana kut̪okana na ut̪amkaji ambayo nriyo shughuli ya Fonolojiya. Tukumbuke tu kuwa /mvit̪a/ ni maneno mawili /mvi + t̪a/ na /t̪/ ya Kimvit̪a yatamkwa /ts/ katika Kimijikenra.

Tukiregeleya Kimijikenra tut̪akwenraona kuwa /tsaka/ ina maana ya 'msitu'. Twangaliye neno 'msitu' kut̪oka lugha nyengine za karibu huitwaje:

/tsaka/	Kimijikenra
/tsaha/	Kingazija
/t̪aka/	Kimvit̪a
/ishaka/	Kit̪ʰikuu
/itsaka/	Kitaita
/badda/	Kipokomo
/katheka/	Kikamba
/mũtitũ/	Kikikuyu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

/esichaha/ Kibaluhya

/osnet/ Kipsigis

/chaka/ Kisanifu

Katika mifano hii, tuṯaona /tsaka/ yenye maana ya ‘msitu’ sauti /ts/ inapatikana katika Kimviṯa, Kingazija na Kisanifu kuṯokana na mageuko yake kama tulivokwishakusema awali. Aidhan, ufafanuzi niliyoupata nyanjani kuhusu ‘shaka’ ni ‘msitu mdogo wa mik^{h}oko uliyojiṯenga kidogo na bara ambao umezungukwa na maji koṯ^{h}e’; ni ṯafauṯi na Kisanifu na Kitaita hurejeleya ‘thicket/bush’. Tumeona kuwa maneno yoṯ^{h}e, juu ya ṯafauṯi za uṯamkaji kama Kipokomo na Kipsigis, yanamaanisha ‘msitu’. Kuṯamkwa /tsaka, tsaha, ṯaka/ ni maana moja ya msitu kwa sababu mageuko ya /h/ kuwa /k/ na kinyumewe katika Kingazija, Kimijikenra na Kiswahili asiliya tuṯaona yanapatikana katika maneno /kondoo, hondoo/ ‘sheep’ na /konde, honde/ ‘kijishamba’. Tukumbuke piya, Ras Ṯaka (ambayo ni Maḏobini) imekabiliyana na Nyali na K^{h}ongoweya ambayo tumesema yamaanisha msitu mkubwa. Sasa basi /mvi + ṯa/ tutaipata kwa kusema kuwa paliṯokeya udonroshaji wa silabi ya mwisho tukabakiwa na /ṯa/ katika jina /mviṯa/. Kuṯokana na uchanganuzi huu twaweza kusema, kwa hivo, /tsa/ na /ṯa/ ni ‘msitu’. Hatimaye**,** /mviṯa/ kwa namna wanavoṯamka wenye lugha ya Kiswahili asiliya ni ‘mji wa msitu’ na wala *si* ‘mji wa vita’ kama ilivozoweleka. Uṯaraṯibu wa uṯafiṯi wetu umeṯanguwa dhana ya kuṯamka jina la mji huu vengine na kweleza usuli wake kivengine.

vi).2 Mambasa ni Mambasah? Yaonekana Mambasa yaweza kuṯokana na Mambasaha /mamba + tsaha/ na ukarekodiwa kama /mambasah/. Dalili ya udonroshaji wa /ha/ wapatikana katika uwandishi wa /mambasa/ kwa Kiyarabu (ممباسة) /mambasah/, yenye ‘ṯa marbuṯah’ ambayo huṯamkwa ‘h’ ukikoma wakaṯi wa kusema. Ushahidi huu uko katika pesa zilizokuwa zikitumika Afrika Mashariki 1888 B.K / 1306 B.H (Numista, 2021).

Kuṯokana na maelezo ya hapo juu tunaweza kusema basi Mambasa piya ni mshikamano wa majina mawili /mamba + sa/ yenye maana ya ‘mwamba/mamba wa msitu’. Jamii ya Kikamba huuwita mji huu /mwambatsa/ na ya Kidawida huuwita /mambasa/ (CASAS, 2012: 12). /mwamba/ na /mamba/ ni moja kwa sababu katika Kiswahili asiliya pahali penye jiwe gumu hupaita /mwamba/ na mnyama wa mt^{h}oni ‘crocodile’ humwita /mwamba/ au /mamba/ pengine kuṯokana na ngozi yake ngumu. Piya Mwambasa kuwa Mambasa, uko mfanyiko huu katika lafudhi (idiolect) ya wat^{h}u kusema ‘Namambiya’ badala ya ‘Namwambiya’. Hivo basi twaweza kusema kiasiliya Mambasa, Mambasah, Mwambatsa, Mwambasa ni alomofu za Mwambasa.

vi).3 Kisauni ni Kiṯaruni: Baada ya kuwona /ts/ ya Kimijikenra ni /ṯ/ au /s/ kwa Kimviṯa tunaweza sasa kusema haṯa /kitsauni/ ni /kisauni/, /kiṯauni/. Kisauni inaṯokana na jina ‘kiṯaruni’ Kimviṯa kwa maana ya kijishamba kijidogo chenye kulimwa mazao machache ya kukidhi haja. Kiṯaru tunaweza kwigawanya kimofu /ki- + -ṯa- + -r- + -u/ ikawa /ki-/ ni kiyambishi ngeli cha udogo (7/8), /-ṯa-/ mzizi wa nomino msitu kama tulivosema awali, /-r-/ kwa Kibantu ina maana ya ukubwa (kwa mfano, katika maneno /mkuru/, /shikiro/, /pura/, /guru/ ambapo tukiidonrosha /r/ maneno hayo yatakuwa /mkuu/, /shikio/, /pua/, /guu/), na /-u/ ni kiishiyo. Hivo, tumeona kuwa /ṯa/ imegeuka kuwa /sa/ katika Kisauni ambayo tulisema ni msitu na /ru/ ni ukubwa kwa hivo ‘msitu mkubwa’ (yaweza kunasibishwa na Ṯaru mji uliyoko 80km kutoka Mambasa) lakini maana imegeuka sasa kiṯaru kumaanisha kijishamba kwa kwingiliwa na /ki/ ya udogo. Tukidonrosha /-ni/ ambayo tumesema ni mofimu ya mahali halafu katika /kiṯaru/ tukidonrosha /r/ tutapata /kiṯau/. Tuliwauliza wasailiwa wetu kuhusu jina la sehemu ya Kiṯau iliyoko Wilaya ya Lamu na sifa za sehemu hiyo tuliyelezewa ni sehemu iliyoko mkabala na kisiwa cha Amu ambako nriko kwenye mashamba ya wat^{h}u wa Amu na Shella; na kila aliyeishi Mambasa siku za kuishi, ajuwa kwamba Kisauni mpaka leo yaitwa ‘shamba’ na wat^{h}u wa ‘mjini’ (kisiwani).

vi).4 Mambasa au Mombasa? Swali laweza kuzuka basi ikiwa ni Mambasa/Mwambasa kefu Mombasa? Kwanza tujuwe kuwa wananchi wa Mkowa wa Pwani ambawo ni wa makamu ya miyaka 50 na kwenreleya huuwita mji huu Mambasa. Zaidi, ni Profesa Rocha Chimerah, mwalimu mzee wangu, mara zoṯ^{h}e ninazozungumza naye mpaka sasa, huutaja mji huu Mambasa, juu ya usomi wake. Hivo basi, Mombasa yaweza kuwa yaṯokana na masikizi ya mwandishi wa jina asiliya la Mwambasa kama ilivorekodiwa Mwali ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

Comoro kuwa Moëli kama tulivotaja katika maelezo ya Nyali. Au, pengine walirekodi, kwa samahani (Taylor, 1891: Dibaji), lafudhi ya mtu fulani kwa sababu kunao wasemaji pwekepweke wanaosema ‘monyewe’ badala ya ‘mwenyewe’ katika lugha ya kikawaida mjini Mambasa.

Tumeona katika sehemu hii kuwa nyusuli za toponimi za mitʰaa ilitegemeya zaidi vitu vinavoonekana dhahiri va kimaumbile. Piya tumeona kuna ṯafauṯi ya uṯamkaji wa majina ya mitʰaa hiyo kwa Kiswahili asiliya na Kisanifu ambacho hakikuhifadhi sauṯi hizi katika haṯi yake. Ṯafauṯi hizo za kuṯamka jina zimetupa ufunuwo wa maana ṯafauṯi ya majina haya. Alakulihali, tumebayanisha na kuthibitisha kuwa etimolojiya ya toponimi za mitʰaa ya kale ya Mambasa ina miyonroko ya kuṯokana na mazingira na maumbile ya mahali hapo.

HIṮIMISHO

Lengo kʰuu la makala haya lilikuwa kuṯowa maelezo ya usuli wa toponimi ya baadhi ya mitʰaa ya Mambasa. Kwa kutumiya uṯaraṯibu wa kuchunguza toponimi kietimolojiya na kutumiya Uṯaraṯibu wa Isimu Mapisi tumeweza kuchanganuwa nyusuli za majina hayo. Sababu ni kwamba dhana iliyojidhihirisha wakaṯi wa uṯafiṯi wetu tulikuta wasailiwa wana maoni ṯafauṯi ṯafauṯi kuhusu asili ya majina ya mitʰaa hii. Tulichaguwa wazee wa miyaka 50 na zaidi ili kupata data ya kimsingi kuhusu uṯamkaji na fasili za maana ya miji hiyo. Tuliyona sampuli ya wasailiwa hawa nriyo sṯahikifu kwa kucheleya kwathiriwa na Kisanifu ambacho hakikuhifadhi sauṯi zoṯʰe za Kiswahili asiliya. Japo mas’ala ya kiisimu-mapisi yana kiwango cha udhahanifu lakini tuliweza kupunguza athari hii kwa kurejeleya maandiko yaliyoko yenye maelezo ya toponimi hizi.

Kuṯokana na Uṯaraṯibu wa Ulinganisho wa visawe kuṯoka lugha kadhaa zinazokurubiyana na Kiswahili: Kimijikenra, Kipokomo, Kingazija, na kwa uchache lugha za Kibantu za bara ya Kenya tumeweza kubainisha kuwa, mwanzo, lugha hizi zina uhusiyano katika ngazi za kifonolojiya, kimofolojiya, na kisemantiki. Pili, athari za kisemantiki piya zimedhihirika katika lugha tulizochanganuliya data yetu na hivo kusakinisha madhumuni yetu kwamba maana za toponimi za mitʰaa ya kale ya Mambasa zaṯokana na maumbile ya mazingira sawiya katika lugha nyengine za Kibantu: Ganjoni, Kaloleni kuṯoka Mambasa, na Kiganjo, Galole, huko Nyeri, Tana River kimṯawaliya. Aidhan, tumefunukiwa kwamba ṯafauṯi za kimaṯamshi ya sauṯi na mageuko yake katika matumizi huleta ṯafauṯi za nyusuli za majina ya mitʰaa ya kale ya Mambasa, kwa mfano, Mviṯa, Kʰongoweya, Mwambasa; sauti /ṯ/ ya Kiswahili asiliya imeṯafauṯisha usuli na maana ya jina la mji huu. Tumefunukiwa piya katika uṯafiṯi huu kwamba mitʰaa ya hivi karibuni imepata toponimi zake kuṯokana na mazingira ya kukurubiyana na jengo (Ngomeni), matukiyo (Baghani), maenreleo mapya katika mji (Kavani), majenzi ya nyumba kimpangiliyo (Majengo), au, ni hisiya za mpaji jina (Kerekeṯa). Makala haya yameleta wazo jipya kuhusu kujenga dhana katika mas’ala ya kiṯamaḏuni, kimapisi, kiisimu, na chimbo za mji wa Mambasa. Kuhusu wazo hili twaweza kusema nini kuhusu toponimi za miji mengine katika Mkowa wa Pwani au Kenya nzima kwa faiḏa ya mapisi ya jamii zetu? Je, uṯafiṯi wetu umefunuwa milango ipi ya tʰafiṯi za usuli wa Waswahili? Haṯimaye, toponimi hizi zawezaje kugeuzwa kuwa bidhaa za kiuṯalii ili zivutiye waṯalii kuṯembeleya miji hii?

SHUKURANI

Nawashukuru ghaya watʰu woṯʰe walonisaidiya wakaṯi wa matayarisho ya makala haya wakiwamo Prof. Rocha Chimerah, PU; Prof. Issa Mwamzandi, UoK; Dkt. Vifu Makoti, MKSU; Dkt. Hamisi Babusa, KU; Dkt. Kalandar Kamalkhan, TUM; Athman Hussein, Mohamed Mwenje, Khalid Kitito, Saadu Hashim, na Mbarak Abdulkadir wote wa NMK; Washairi Hassan Morowa na Abḏilaṯif Abḏalla; na Wanafunzi wangu woṯʰe, kwao wao nawaṯunukiya makala haya.

MAREJELEO

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th century Swahili popular poetry*. Kenya Literature Bureau.

Antilla, R. (1989). *Historical and comparative linguistics*. John Benjamins Publishing Company.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

Bynon, T. (1977). *Historical linguistics*. Cambridge University Press.

Campbell, L. (1998). *Historical linguistics: An introduction*. Edingburgh University Press.

Centre for Advanced Studies of African Society, (2012). *A unified orthography for Bantu languages of Kenya*. Monograph no. 249.

Helander, K. R. (h.t.). Renaming indigenous toponymy in official use in light of contact onomastic theories. Sami University College, Norway.

Hiistoriya, (2020, Jul 12). Who are the Swahili? [video file]. Imetolewa https://www.youtube.com/watch?v=pghUezn9FE4

Karama, M. R. (2021, June). Kugeuza d̪ira ya toponimi ya 'Swahili'. *The University of Kabianga Newsletter 1*(5), 8-9.

Kindy, H. (1972). *Life and politics in Mombasa*. East African Publishing House.

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. Trubner & Co.

Kresse, K. (2007). *Philosophising in Mombasa: Knowledge, Islam and intellectual practice on the Swahili coast*. Edinburgh University Press.

Makoti, V. S. (2007). Digo anthroponymes: Meaning and significance. *Maarifa: A Journal of Humanities and Social Sciences 2* (1) 18-28.

Mazrui, A. A. (2012). *What's in a name?: European imperialism and the re-naming of Africa*. Kandi ya A. Mazrui, State University of New York at Binghamton, New York.

Mindat.org. (2021, June). *Ras Iwetine, Mombasa, Kenya*. Ilisomwa kutoka https://www.mindat.org/feature-196036.html .

Mohamed, M. A. (2001). *Modern Swahili grammar*. East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu alipofufuka*. Jomo Kenyatta Foundation.

wa Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziyya*. TUKI.

Mutua, M. (2021, June 20) It's time to decolonise Kinyaa. *Nation.Africa*. Ilisomwa kutoka https://nation.africa/kenya/blogs-opinion/opinion/it-s-time-to-decolonise-kinyaa-3443516

Mwalonya, J., Nicolle, A., Nicolle, S. & Zimbu, J. (2004) *Mgombato: Digo-English- Swahili dictionary*. Bible Translation Literacy.

Numista, (2021, June 2). IBEA coinage.

Ilisomwa kutoka https://en.numista.com/catalogue/pieces8981.html

Nurse, D. & Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the history and language of an African society 800-1500*. University of Pennsylvania Press.

Nzasu, J. & Odongo, W. (2014). *Our county: Mombasa*. Oxford University Press.

Owino, S. (2019, October 27). What's in a name? Take heed in these legal views, implications. *Kenyan Digest*. https://kenyandigest.com/whats-in-a-name-take-heed-in-these-legal-views-implications/

Rose-Redwood, R., Alderman, D. & Azaryahu, M. (2010). Geographies of toponymic inscription: New directions in critical place-names studies. *Progress in Human Geography 34*(4), 453-470.

Sacleux, C. S. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Institut d' Ethnologie.

Stigand, C. H. (1915). *A grammar of dialectic changes in the Kiswahili language*. Cambridge University Press.

Taylor, W. E. (1891). *African aphorisms*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Tent, J. & Slatyer, H. (2009). Naming places on the Southland: European place-naming practices from 1606 to 1803. *Australian Historical Studies 40*(1), 5-31.

Tent, J. (2015). Approaches to research in toponymy. *Names 63*(2), 65-

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.368

74. https://doi.org/10.1179/0027773814z.000000000103 .

Walsh, M. T. (2003). Hunter-gatherers in the hinterland of Mombasa: Notes on the Maumba of Chonyi and related traditions. *Notes*.

Wamitila, K. W. (1999). What's in a name: Towards literary onomastics in Kiswahili literature. *AAP 60*, 35-44.

Wanjiru, M. W. & Matsubara, K. (2017). Street naming and the decolonisation of the urban landscape in post-colonial Nairobi. *Journal of Cultural Geography 34*(1), 1-23. https://doi.org/10.1080/08873631.2016.1203518.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.